

CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM

S.L.P. 35091 • DAR ES SALAAM • TANZANIA



TAARIFA KWA UMMA

MAHAFALI YA 51 YA CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Kampasi ya Mwalimu Julius Nyerere, Mlimani, kinapenda kuwataarifu wadau wa Chuo na umma kwa ujumla kuwa kitafanya **Mahafali ya Hamsini na Moja (51)** duru ya pili na ya tatu ya **siku ya Jumamosi, tarehe 16 Oktoba 2021 na Jumatano, tarehe 20 Oktoba 2021** katika Ukumbi wa Mikutano wa Mlimani City, kuanzia saa nne asubuhi.

Duru hizi ni kwa minajili ya kutunuku Shahada za Awali, Stashahada na Astashahada kwa wahitimu wote waliofaulu na kumaliza masomo yao katika mwaka wa masomo 2020/2021 kama ifuatavyo: Katika Duru ya Pili itakayofanyika **Jumamosi tarehe 16 Oktoba 2021** watahudhurishwa wahitimu kutoka Ndaki ya Uhandisi na Teknolojia (CoET); Ndaki ya Insia (CoHU); Ndaki ya Teknolojia za Habari na Mawasiliano (CoICT); Shule Kuu ya Madini na Jiosayansi (SoMG); Shule Kuu ya Biashara (UDBS); na Taasisi ya Taaluma za Kiswahili (IKS). Katika Duru ya Tatu itakayofanyika **Jumatano tarehe 20 Oktoba 2021** watahudhurishwa wahitimu kutoka Ndaki ya Sayansi za Kilimo na Teknolojia ya Chakula (CoAF); Ndaki ya Sayansi Asilia na Tumizi (CoNAS); Ndaki ya Sayansi za Jamii (CoSS); Shule Kuu ya Uchumi (UDSoEC); Shule Kuu ya Sayansi Akaa na Teknolojia ya Uvuvi (SoAF); Shule Kuu ya Sheria (UDSoL); Shule Kuu ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano ya Umma (SJMC); na Taasisi ya Taaluma za Maendeleo (IDS). Duru ya Tatu itafanyika tarehe 20 Oktoba 2021 badala ya tarehe iliyokuwa imepangwa awali ambayo itakuwa ni sikukuu ya Maulid.

Katika duru zote mbili kutakuwa na jumla ya wahitimu **4,298**. Kati yao **4,121** watatunukiwa shahada za Awali na 177 watatunukiwa stashahada na astashahada.

Mchanganuo wa wahitimu kwa tuzo husika ni kama ifuatavyo:

TUZO	ME	KE	JUMLA	% KE
Shahada za Awali (<i>Bachelor Degrees</i>)	2,201	1,920	4,121	46.6
Stashahada na Astashahada (Non Degrees)	124	53	177	29.9
JUMLA	2,325	1,973	4298	45.9

Aidha, mahafali haya ni mojawapo ya shamrashamra za kuadhimisha miaka 60 tangu Chuo kuanzishwa mwaka 1961. Uongozi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam unawakaribisha wadau wote wa elimu ya juu kuhudhuria mahafali haya muhimu katika historia ya chuo chetu. Pia mahafali haya yatarushwa mubashara kupitia vyombo vya habari vya Mlimani na mitandao ya kijamii.

Imetolewa na

Prof. William A. L. Anangisye
Makamu Mkuu wa Chuo
11 Oktoba 2021

Simu ya Moja kwa Moja: +255 22 2410751
Simu ya mezani: +255 22 2410500-8

CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM
Barua Pepe: relation@admin.udsm.ac.tz